METROPOLITAN JOURNAL OF SOCIAL AND EDUCATIONAL RESEARCH
ISSN: 1813-4270
Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44

# USAWIRI WA JINSIA YA KIUME KATIKA RIWAYA YA MSURURU WA USALITI

1 Karuhanga Deusdedit, 2 Dr. Beverlyne Asiko Ambuyo
1, 2 Metropolitan International University

## IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa jinsia ya kiumme katika riwaya ya Msururu wa usaliti. Mtafiti alichanganua taswira ya mwanamme katika riwaya ya Msururu wa usaliti. Kuchanganua taswira za mwanamume katika Riwaya ya Msururu wa usaliti na Mwenda Mbatiah na ile ya jamii ya kiafrika, Kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke kimamlaka katika Riwaya ya Msururu wa usaliti., Kubainisha namna tamaduni na itikadi za kijadi zinavyochangia hulka ya mwanamme katika jamii ya Msururu wa Usaliti. Nadharia ya ubabe- dume iliyotokea miaka ya 1980 kupitia maaandishi ya John Gray itatumiwa. Mihimili ya itikadi za jamii, uwezo na uongozi pamoja na utamaduni ndizo zilizotumiwa katika utafiti huu.Utafiti huu ulishughulikia kazi ya Msururu was usaliti, riwaya yake Mwenda Mbatiah. Riwaya hii imechaguliwa kwa sababu ina wahusika wengi wa kiume na kike wa umri, tabaka, viwango vya elimu tofauti na kadhalika ambao wanajitambuliza na kutambulishwa na jamii tofauti tofauti. Muundo wa kimaelezo ulitumwa katika utafiti huu. Riwaya ya Msururu wa Usaliti ilisomwa ili kupatata deta. Deta iliyofanyiwa utafiti ni ile deta tu inayoshughulikia taswira ya mwanamme.Sehemu zingine riwayani hazitashughulikiwa. Deta iliyokusanywa ilinakiliwa kisha baadaye kuchanganuliwa kwa kutumia uchaganuzi wa kiuthamano ambapo programu ya SPSS ilitumiwa. Uchanganuzi uliongozwa na madhumuni ya utafiti.Utafiti huu utachangia katika kuweka msingi wa kuchanganua riwaya ya kisawhili kitaaluma kwa kujikita kwenye kipengele cha jinsia na mamlaka hasa mamlaka ya mwanamme dhidi ya mwanamke. Kazi hii itakuwa mwongozo kwa waandishi wa baadaye wa riwaya ya Kiswahili kuandika kazi nzuri kuhusu jinsia ya

kiume kwa kurejelea jamii Fulani. Vilevile utafiti huu utasaidia wasomi kuelewa taswira mbalimbali za mwanamme na jinsi picha hizi zinavyomwathiri mwanamke.

**Usuli wa Mada**

Riwaya ni mojawapo wa tanzu za fasihi andishi ambayo ni utungo mrefu wenye wahusika wengi na unaotungwa kwa njia ya masimulizi. Fasihi andishi ni aina ya fasihi inayosambazwa na kuhifadhiwa kwa njia ya maandishi kwa mfano, riwaya, tamthilia, mashairi, hadithi fupi na kadhalika. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa njia ya ubunifu kuelezea masuala mbalimbali yanayomuhusu binadamu na mazingira anamoishi. Na fasihi hugawika katika aina kuu mbili ambazo ni fasihi andishi na fasihi simulizi.

Suala la uana limepewa kipaumbele miongoni mwa masuala yanayotafitiwa katika taaluma mbalimbali zinazohusu maisha ya binadamu. Majukumu ya jinsia ya kike na jinsia ya kiume ni suala ambalo linaendelea kuzua mgogoro miongoni mwa watu wa jamii mbalimbali. Tafiti nyingi zilizopo zimeshughulikia masuala ya kike. Kuna haja ya utafiti kufanywa kuhusu suala la jinsia ya kiume katika fasihi

Mwanamme kote duniani amepewa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Chanzo cha tofauti hii kulingana na Engles (1975) ni migawanyiko ya utabaka. Anaeleza kwamba wanajamii walikuwa wakiishi maisha ya ujamaa. Mabadiliko yalipotokea kukazuka mfumo wa ubabedume ulioanza kutawala mahusiano yote ya jamii. Mfamo huu ulikolea wakati kazi za waume kama ufugaji zilianza kuleta faida kuliko kazi za wanawake za nyumbani. Kulingana na Engels (Ibid), huu ndio ulikuwa mwanzo wa mwanamke kumtegemea mwananmme katika uhusiano wote wa jamii hasa wa kiuchumi. Hivyo mwanamke kuwa na hadhi ya chini huku mwanamme akiwa na hadhi

METROPOLITAN JOURNAL OF SOCIAL AND EDUCATIONAL RESEARCH
ISSN: 1813-4270
Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44

ya juu, mshawasha huu ndio unamfanya mtafiti kuchunguza kama hali hii inajitokeza katika riwaya ya Msururu wa Usaliti.

Kuhusu ulimwengu unaotawaliwa na wanaume Dehlerup (1987) anasema, ubabedume ni hali ambapo nafasi zote za utawala au uongozi na uamuzi ziko mikononi mwa wanaume yaani ni hali inayomwangalia mwanamke kama mtawaliwa na mwanamme kama mtawala.Katika utafiti huu mtafiti aliangalia hali inavyojitokeza katika riwaya ya Msururu wa usaliti. Nafasi kama vile za kisiasa kuchumi, viwandani, kidini na kijamii ambamo idadi kubwa ya nafasi za juu katika uongozi zinachukuliwa na wanaume. Bila shaka hali kama hizi zinamwacha mwanamke katika mashaka. Hiyo basi, utafiti huu ulijaribu kuangalia kama hali hii inadhihirika katika riwaya ya Msururu wa Usaliti.

Moi (1985), anasema kwamba mwanamme ana sehemu ya maumbile yake ambayo ni dhahiri – uume na mwanamke hana. Freud anapomwangalia mwanamke haoini thamani yoyote kwake.Tofauti ya kimaumbile ya mwanamke na mwanamme imeangaliwa kama chemichemi ya ukinzano wa kimawazo na hatimaye kusababisha tofauti katika majukumu ya kijamii. Hali hii inampa mamlaka mwanamme dhidi ya mwanamke na kwa njia moja au nyingine kumdunisha mwanamke. Mfafiti alijaribu kutathmini ikiwa hali hii inajitokeza katika jamii ya mwandishi wa Msururu wa Usaliti.

Maclennes (1998) anabainisha jinsi ambavyo masharti ya kihistoria na ya kitamaduni yanavyo halalisha mielekeo na mitazamo tofauti baina ya jinsia ya kike na kiume. Anaelezea kuwa udume hauwezi kubainishwa kama sifa ya mwanamme bali hutokana na itikadi na utamaduni wa jamii husika. Masharti mahsusi ya kihistoria yanayodhibiti imani za mme na mke katika jamii na majukumu yao tofauti huendelezwa kupitia kwa imani za kijamii, matarajio na mielekeo yao.Utafiti huu unanuia kupata ukweli wa usemi huu. Riwaya ya Msururu wa usaliti ya Mwenda Mbatiah ilishughulikiwa.

Mwandishi Mwenda Mbatiah, anasimulia maisha ya jinsia mbili yaani ya kike na ya kiume. Anadhihirisha jinsi, jinsia ya kiume inavyodhulumu ile ya kike katika shughuli mbalimbali. Pia, katika kazi yake, anagusa sana utamaduni wa kiafrika ambao mwanamume huchukuliwa kama kiumbe hodari, mwenye uwezo, mamlaka zaidi, dhidi ya mwanamke . Mwenda Mbatiah anadhihirisha jinsi Mhsika Kage kiongozi hodari wa kike, mwenye busara, maarifa na msimamo thabiti anavyokandamizwa na kudharauliwa na mwanamme. Itikadi na mikoo ya kiaafrika imemnyima haki zake faafu kimaumbile mwanamke, chakula kilicho bora ni cha mwanamme maana jinsia ya kike huchukuliwa kuwa duni katika majukumu, sifa na nafasi ya mwanamume katika riwaya hii. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ubabedume inayosisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiuma katika jamii za kiaafrika. Mwenda Mbatiah anamsawiri mhusika huyu Kage akijitahidi kuchomoza kichwa katika shughuli za jamii kama vile siasa na hali yoyote inayohusika na mamlaka au cheo. Kage ni msichana mwenye msimamo thabiti, kwake anaamimi kwamba mtu yeyote aliye hai ana uwezo wa kutumia ubongo wake kujipatia mali kwa njia halali. Wazazi wake wanataka mtoto ajiunge na chuo kikuu cha Chuki na kuisoma kozi ya utabibu lakini kwake anataka kusoma kozi ya mazingira. Kunajitokeza mgogoro wa wazazi dhidhi ya mwanao wa pekee lakini hatimaye kage anafaulu anachukuwa kozi aliyoitaka.Chuoni,anachaguliwa kama kiogozi wa mazingira. Anajaribu kuhifadhi mazingira lakini fikra zake kama kiongozi wa kike hazitambuliwi ila zinadunishwa na jinsia ya kiume hadi anapigwa risasi mguuni na kuchukuliwa hospitalini ishara kwamba jinsia ya kike haina mamlaka,mwenye mamlaka ni mwanamme.

Mtafiti alishughulikia riwaya ya Msururu wa Usaliti hasa kwa kuchambua na kuweka wazi taswira za mwanamme katika Riwaya ya Msururu wa usaliti, uhusiano wa mwanamme na mwanamke katika nyenzo za kimamlaka na namna utamaduni na

itikadi za kijadi zinavyochangia hulka ya mwanamme katika jamii ya Msururu wa usaliti.

## Suala la Utafiti

Swala la jinsia limetafitiwa na watafiti wengi. Tafiti nyingi za hapo awali zimeegemea zaidi kwenye aina ya dhuluma wanazokumbana nazo wanawake katika jamii za kiafrika kwa ajili ya mamlaka mwanamme anayopewa na jamii husika dhidi ya mwanamke. Aidha tafiti hizo zinaonyesha kuwa mwanamke anaendelea kudhulumiwa na mwanamme, lakini nyingi hazionyeshi picha mbalimbali za mwanamme na jinsi picha hizo zinavyomwathiri mwanamke katika jamii za kiafrika. Eneo hili limeonekana kupuuzwa na watafiti wengi wa fasihi ya Kiswahili. Watafiti wengi wameshughulikia jinsia ya kike, jinsia inayopambana kutetea haki zake na kupuuza kuishughulikia ile ya kiume ambayo inaingiliana kwa njia moja au nyingine na ya kike. Jinsia hizi pia zinaingiliana na kukamilishana kwa namna moja au nyingine. Tafiti zinazoshughulikia taswira mblimbali za mwanamme na jinsi taswira hizi zinavyomwthiri mwanamke hazijafanywa na ndio kusudi la utafiti huu.

## Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo;

(i) Kuchanganua taswira za mwanamume katika Riwaya ya Msururu wa usaliti na Mwenda Mbatiah na ile ya jamii ya kiafrika.

(ii) (ii) Kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke kimamlaka katika Riwaya ya Msururu wa usaliti.

(iii) Kubainisha namna tamaduni na itikadi za kijadi zinavyochangia hulka ya mwanamme katika jamii ya Msururu wa Usaliti.

## Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia-tete zifuatazo;

i) Taswira ya mwanamume katika Riwaya ya Msururu wa usaliti na Mwenda Mbatiah si ya ukandamizaji, bali inamjenga mwanamke katika majukumu yake katika asasi za mamlaka.

ii) Riwaya ya Msururu wa usaliti ina mwongozo bora katika uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika mamlaka.

iii) Utamaduni na itikadi ni kigezo muhimu katika kuimarisha mamlaka na ni mwongozo katika riwaya ya Msururu wa usaliti.

## Umuhimu Wa Utafiti

i) Utafiti huu ulichangia katika kuweka msingi wa kuchanganua riwaya ya Kiswahili kitaaluma kwa kujikita kwenye kipengele cha kufafanua taswira ya mwanamume na jinsi taswira hizi zinavyomwathiri mwanamke.

ii) Kwenye utafiti huu mtafiti alichunguza mamlaka katika nyenzo mbalimbali za jamii kama vile ndoa, siasa na utamaduni katika kuwasilisha ujumbe mbalimbali wa mwandishi kwa lengo la kuzindua. Hivyo basi kazi hii itakuwa kama mwongozo kwa waandishi wa baadaye wa riwaya ya Kiswahili kuandika kazi nzuri zaidi kuhusu taswira ya mwanamme kwa kurejerea jamii fulani.

iii)Lengo la uhakiki ni kudhihirisha kusudi la mtunzi kwa kuondoa vikwazo vyovyote ambavyo

vyaweza kutatiza uelewaji. Kwa jumla utafiti huu ni muhimu kwa wasomaji wa riwaya.Utawawezesha kuelewa kwa nini msanii akasawiri uhalisia wa jinsia ya kiume vile katika riwaya ya msururu wa usaliti.

iv)Wasomaji wanaweza pia kufahamu ufundi aliotumiwa katika uchoraji wapicha za mwanamme ili kutekeleza jukumu la kuwasilisha ujumbe kwa nia ya kuzindua na kusisimua wasomaji wake.

v) Aidha, kwa sababu nitaangalia ubabedume kitaaluma kwa kutumia misingi ya kinadharia, utafiti huu utampa msomaji mshawasha wa kusoma upya kazi hii ya Mwenda Mbatiah.

vii)Umuhimu wa kutumia mbinu ya mamlaka katika kazi ya fasihi ni kusawiri mawazo ya mtunzi kwa kina kirefu zaidi kwa sababu matumizi ya kipengele cha mamlaka humpa msomaji au mtazamaji viwango vingi vya ufasiri na ufahamu. Matumizi ya mamlaka ya kijinsia hulenga kufikia maana mpya, pana na ya kipekee kwa kutumia mbinu ya uhamisho. Hivyo, utafiti huu utabaini ikiwa Mwenda Mbatiah amefikia malengo haya.

viii) Nimesema katika sehemu ya usuli kuwa, kazi za kiuchambuzi na uhakiki zilizowahi kutokea
kuhusu riwaya hii ya Msururu Wa Usaliti hazijashughulikia jinsia kama mada
mahsusi. Tahakiki za kitaaluma zilizowahi kutokea zimehusu hasa maudhui (Vunyoli, 2004),
wahusika (Kisurulia, 2000), mtiririko wa hadithi (Wamitila, 1998), taswira (Musembi, 2008) na utabaka(Arinaitwe2018.)

ix)Utafiti pia utaweka misingi ya kuhakiki riwaya za Kiswahili kitaaluma hasa tukizingatia jinsia

x).Utafiti katika uwanja wa fasihi ni njia mojawapo muhimu ya kuikuza na kuhifadhi lugha. Hii hutokana na msamiati thabiti wa kiuchambuzi unaotokana na nadharia mbalimbali za fasihi.

Aidha, dafina ya maandishi ya Kiswahili inakuwa kubwa mbali na kuipa hii lugha msamiati mgeni au kuimarisha istilahi zilizopo za kifasihi na za kiuchambuzi.

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ubabe-dume.

**Nadharia ya Ubabe-dume**

Nadharia hii ilitokea katika miaka ya themanini (1980) kupitia kwa maandishi ya John Gray. Msimamo wake kuhusiana na swala la uana uliwafanya wanasikolojia kutambua umuhimu wa kuchunguza uwezo wa mwanamume na mwanamke katika jamii kupitia kwa nyanja zifiatazo:

i) Mfumo wa uongozi katika jamii.

ii) Migao ya majukumu kati ya mwanamme na mwanamke.

iii) Mpangilio wa jamii kijinsia na sababu za mpangilio huo.

Nadharia ya ubabe-dume inabainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Dhana "Mwanamume" ipo kwa misingi ya kibayolojia ilhali "uume" hutokana na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii. Ni kutokana na kauli hii ambapo Walsh (1997) anaeleza kuwa, uume hubainika wazi kwa misingi ya ushari, ushindani na uwezo wa kutawala, kuamuru na kuzuia. Katika jamii za kiafrika "uume" uhusishwa na uwezo wa mwanamume kuwa na mafanikio, kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Kwa hivyo umme huzaliwa na kutukuzwa na utamaduni, na huhalalishwa kwa njia, hali na nyakati tofauti za jamii nzima.Sura ya mwanamume na mvulana katika jamii haitokani na vile wanavyojifikiria bali hujengwa kutokana na matarajio ya kiitakadi na kitamaduni. Ni kipitia kwa matarajio haya ambapo baadhi ya sifa kama vile

stahamala, ubabe na ukatili, katika kutenda bila kujali iwapo vitendo hivyo vinaweza kuleta maangamizi au vurugu katika jamii husisitizwa.

Asili ya nadharia hii hufungamanishwa na dhakari na wenye kuimiliki (waume). Wao huchukuliwa kuwa na nguvu, wenye kuheshimiwa, na kustahibiwa katika jamii. Bindamu anayezaliwa na kiungo hiki huchukuliwa kama raslimali yenye manufaa makubwa kwa jamii. Hivyo basi siku zote wenye dhakari hupewa hadhi ya juu na huchukuliwa kuwa bora zaidi ya wanawake ambao hawana kiungo hiki. (Izugbara, 2005).

Mtajwa (2005) anaeleza kuwa, itikadi za kitamaduni ambazo hubainisha aula, uwezo, nguvu, uhodari na uhayawani wa mwanaume, kielezo chake cha mamlaka, utendakazi wa viungo vya uzazi, upenyezi wa dhakari, kuwa na uhasiano wa kingono na zaidi ya mwanamke mmoja nje ya ndoa, ushari wa kimapenzi, sauti nzito miongoni mwa sifa zingine, huchukuliwa kama sifa mwafaka zenye kumtambulisha mwanamume kinyume na wasomiliki dhakari (wanawake). Anazidi kufafanua kuwa, dhakari hutumika kama chombo cha kumshusha hadhi mwanamke. Kwa sababu hii dhakari ni asili ya uanaume, silaha ya kumwezesha mwanamume kuwa mshindi katika ushindani wa kijinsia.

Maana yake na umuhimu wake huhalalishwa katika tendo la ngono na sifa zake muhimu zenye kuakisi matarajio ya jamii juu ya mwananmume. Anazidi kusema kuwa, katika kuzaliwa kwa mtoto, watu huangalia kwa makini kuwepo au kutokuwepo kwa dhakari. Jambo ambalo hutokea katika fikra za kitamaduni za wanajamiii kuwaweka watoto wa kiume katika kategoria mahsusi kama ulivyo mtazamo wa utamaduni wa jamii husika. Wasiomiliki kiungo hiki hujamiishwa kwa njia tofauti yenye kuafiki nafasi yao katika jamii. Ni kupitia kwa mtazamo huu ambapo wanasosholojia hukubaliana na msingi huu wa nadharia hii katika kumpa mwanamme uwezo anaomiliki katika jamii. Utambuzi wa uume na uke hujengwa miaka ya awali ya mtoto. Takribani katika umri

wa miaka miwili, watoto huanza kuelewa utambulisho wao wa kijinsia. Hivyo, kadri watoto wanavyokua, huanza kuepuka matendo na shughuli ambazo huaminiwa kutoafikiana na jinsia yao.

Uhusiano wa kiuwezo wa kijinsia umeacha hiba kwa vile ambavyo mwanamume humiliki uwezo mkubwa katika raslimali za jamii, fadhila na katika kuamua juu ya maswala muhimu ya kijamii. Mwanamume huwa na haki zaidi ya mwanamke katika nyumba na maswala muhimu mengine ya umma. Kama izugbara (2005) anavyowanukuu Berger (1995), mwanamume hazaliwi na uume kama sehemu ya viungo vya uzazi bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni wa jamii anamokulia. Kwa hivyo, nadharia hii huchukulia utamaduni kama uti wa mgongo wa misingi yake. Wao hawazingatii maswala ya kibayolojia na kianthropolojia ambayo hushikilia mtazamo kwamba, tabia za kiume ni uhalisia wa maisha ya jamii. Hii ndio maana anasema kuwa, tofauti za kibayolojia kati ya mume na mke hazitoshi kumfanya mwananmme kuwa na uwezo mkubwa, mkware, mbakaji, mwenye mamlaka yaliyokithiri na muuaji, bali utamaduni na mazingira anamokulia huwa na mchango mkubwa.

Nadharia ya ubabedume hufafanua sifa mahsusi mwanamume anajitahidi kuwa nazo (Kimmel 2000). Nadharia hii hujengeka mintarafu katika uwezo na mafanikio. Uwezo wa kijinsia ambao hufafanaliwa na kubainishwa kwa njia tofauti ni kipengele muhimu cha mtazamo wa nguvu za jinsia ya kiume.

Kwa muhtasari, nadharia hii imejikita katika mambo manne muhimu ambayo hutawala matarajio na mielekeo ya jimii kuhusu mwanamume, nayo ni;

i) Itikadi za jamii

ii) Uwezo na ungozi

iii) Utamaduni

iv) Mazingira

Hivyo basi nadharia hii itakuwa mwongozo imara katika kutathmini na kutolea kauli jinsi mwanamume amesawiriwa katika riwaya ya Msururu wa Usaliti. Nadharia hii hutambua umuhimu wa utamaduni, mielekeo na mitazamo ya kijamii kuhalalisha uwezo anaoumiliki mwanamnmme katika jamii.

**MAELEZO YA ISTILAHI**

Dhakari – sehemu ya uzazi wa mwanamume

Uanaume – hali ya kuwa mwanamume

Ubabadume – ushujaa wa mwanamme

Ushari – ufanyaji wa mambo ya kuudhi wengine

Taswira-jinsi mtu anavyoweza kuchorwa na kuweza kutoa picha kamili ya anavyoonekana.

## MBINU ZA UTAFITI

### Utangulizi.

Sehemu hii itashughulikia muundo wa utafiti, vifua vya kukusanya deta, mbinuza kukusanya deta, utaratibu wa utafiti pamoja na uwasilishaji.

### MUUNDO Wa Utafiti.

Muundo wa kimaelezo utatumiwa katika utafiti huu. Muundo huu wa utafiti utakuwa mwafaka kwa sababu utafiti huu ni wa kimaelezo. Aina hii ya utafiti itakuwa bora kwa sababu huu ni utafiti wa uchunguzi. Deta zitaelezwa jinsi zilivyo bila kubadilisha vibadala.

METROPOLITAN JOURNAL OF SOCIAL AND EDUCATIONAL RESEARCH
ISSN: 1813-4270
Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44

**Uteuzi Wa Vifaa VyaKukusanya Deta.**

Mtafiti atateuwa vifaa vitakavyomwezesha kupata deta. Kabu (1987) anasisitiza juu ya kutumia nyenzo au vifaa vya kukusanya data ambavyo ni vya muhimu sana kwa utafiti. Kwa mujibu huu, mtafiti atatumia kalamu na karatasi kwa ajili ya kuandika kuambukumbu muhimu zitakazo patikana wakati wa kusoma matini.

**Mbinu Za Kukusanya Deta.**

Scale (2012) na silver (2010) wanasema kwamba zipo mbinu mbalimbali za kukusanya data na katika mbinu hizo hakuna mbinu inayojitosheleza katika mazingira yake. Mbinu ya usomaji matini kwa kusoma kitabu teule cha Msururu wa Usaliti itatumiwa. Deta itakusanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti.Deta itakuwa usawiri wa jinsia ya kiume katika riwaya. Pia tasnufu zenye uhusiano na mada ya mtafiti zitasomwa. Data ambayo itakuwa nguma kupatikana maktabani itatafutwa kwa kutumia tovuti.

**Utaratibu wa Utafiti.**

Mtafiti ataanza utafiti wake kwa kuandaa malengo yake ya utafiti kulingana na maswala ya utafiti. Kisha atasoma matini yenye uhusiano na mada yake. Sehemu riwayani zinazoonyesha taswira ya mwanamme ndizo zitshughulikiwa. Sehemu nyinginezo hazitashughulikiwa. Mtafiti atakusanya data inayohusiana na mada yake kwa kutumia vifaa alivyoviteua. Data itakayokusanywa itachanganuliwa kwa kutumia uchanganuzia wa kithamano ambapo programu ya SPSS itatumiwa, uchanganuzi utaongozwa na madhumuni.

**Uwasilishaji Na Uchanganuzi Wa Deta.**

Data itakayo patikana itawasilishwa kwa njia ya maelezo baada ya kuchanganuliwa.

**Taswira ya wa Mwanamume katika Riwaya ya Msururu wa Usaliti.**

Mwanamume husawiriwa kwa namna tofautitofauti katika kazi za fasihi huku baadhi ya watunzi wakimsawiri mwanamume katika hali hasi na wengine wakimsawiri katika hali chanya. Usawiri hasi juu ya mwanamume unafanywa kwa makusudi kutokana na mfumo dume ambao upo katika jamii ambao humuona mwanamume kama kiumbu chenye umuhimu na uhodari tele zaidi ya mwanamke katika jamii yoyote. Mfumo dume humuona mwanamume kama kiumbe mwenye uwezo wa kuwa na maamuzi sahihi ya kufanya jambo bila ya kusaidiwa na mwanamke. Athari hii inajitokeza katika kazi nyingi za fasihi ingawa hivi karibuni kumekuwa na jitihada za kuiondoa mtazamo wa mfumo dume dhidi ya mwanamke.

Riwaya ya Msururu wa Usaliti ni miongoni mwa kazi za fasihi ambazo zinamsawiri mwanamume katika nafasi mbalimbali kama ilivyowasilishwa katika sehemu ifuatayo.

**Mwanamume Kama Msaidizi**

Kimaumbile, mwanamume ni mwenye nguvu kwa hiyo hutia jidihada tele katika ufanikaji wa familia yake yaani mkewe, watoto na kila anayeishi katika familia hiyo. Dhana hii imekuwa ikizunguka katika akili ya baadhi ya wanawake hata wanashindwa kufanya maamuzi muhimu katika maisha yao kwa kutia imani katika mabwana zao kuwa ndio watoleao kila mahitaji ya nyumbani yaani chakula, ulinzi, matibabu,ada za watoto, malazi, mahitaji nakadhalika. Mwandishi katika Msururu wa Usaliti ameisawiri hali hii pale anaposema:

Ndipo Mbogo alipomtambua Makena-Bintiye Chifu! Mbogo alichanganyikiwa lakini akajikaza kuthibiti hisia zake na kukamilisha kitendo cha uokoaji alichokuwa ameanza. Alishika makena mikono yote miwili na kujaribu kumwinua. Alipomwachilia, alipomoroka karibu aanguke. Wazo la kumbeba kama mtoto likamjia mbogo. Haikuwa kazi kwake (Uk 61).

Dondoo hili linathibitisha kwamba mwanamume ni msaidizi maana ana uwezo na nguvu za kumsaidia mwanamke. Hapo ni wakati ambapo Makena aliposhambuliwa na mbwa wake Njenge ambaye ni mmojawapo wa majilani wakamraruararua taratibu

lakini punde si punde akasaidiwa na Mbogo. Ilhali suala la mfumodume utawala akili za jamii ya kiafrika wanawake, wanaume nao limewatawala kwa kuwa wanafahamu uwajibu wanaotarajiwa kutekeleza. Mwanamume yeyote anayekosa kutekeleza uwajibu huu hudharauliwa na kudunishwa katika jamii kwani amevunjaa mila na desturi jambo ambalo huchukuliwa kuwa la aibu sana katika masikio ya kila mwanajamii. Pia, mwanamume hujiona kuwa medharauliwa akinyimwa nafasi ya kutekeleza uwajibu wake kwamfano katika dondoo lifuatalo Mbogo hapendezwi na hatua ya bintiye Kage kukataa msada au ufadhili wa pesa aliompa.

Kage alijiwa na wazo la kumlipa babake ule mkopo aliochukuwa kununua gari. Alipompigia simu na kugusia jambo hili, babake alikariri msimamo wake "Hapa sio Uzunguni ambapo baba na mtoto hukopeshana pesa, kwa sababu uhusiano wetu sio wa kibiashara". Kaage hakushangazwa na maneno haya. Alikuwa ameyazoea mahubiri ya babake juu ya Uafrika.Lakini aaliridhika kwamba alikuwa amefanya wajibu wake kuhusu ule mkopo.

Kulingana na maneno haya, Mbogo ambaye ni babake Kage anadhihilisha kwamba kulingana na utamaduni wa kiafrika, lazima baba wa mtu atekeleze uwajibu wake sio kama vile Uzunguni ambapo mtoto hukopeshana pesa na baba mzazi. Kwa hiyo, mwanamume amesawiriwa kama msaidizi anayeutoa bila kutarajia zawadi yoyote bali kama mmojawapo wa uwajibu anaotarajiwa kuutimiza.Kwake kage anataka kumrudishia pesa babake kama alivyokuwa amepata mkopo wa benki lakini babke Mbogo hakupendezwa na msimamo wake Kage maana amemwingilia uume au ufuhali.

Maneno haya yanaonyesha bayana kuwa katika jamii kuna hali ya mwanamume kufanya uamuzi wowote anaoutaka katika ndoa au familia. Kinachomzuia Mbogo kumwoa mke wa pili si makubaliano yake na mkewe Makena, bali ni hofu ya kupoteza kiti chake cha Ubunge juu ya vita alivyotarajia kutoka kwa makanisa. Katika dondoo hili, mwandishi amezingatia itikati na utamaduni wa kiafrika kiasi kwamba,

mwanamume amesawiriwa kama mdikteta hasa katika masuala ya uamuzi, maana nafasi ya mwanamke ni duni katika jamii.

Usawiri huu wa mwanamume hujitokeza katika desturi za kiafrika kwa jumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajiriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo  Kungelikuwa usawa wa jinsia kimamlaka, jinsia zote zingetekeleza uwajibu wa mahitaji ya familia, lakini imaani ya mwafrika haiwezi ikabadilishwa vile ilivyokuwa ndivyo ilivyo hata ndivyo itakavyokuwa, mume hubaki mume hata akiwa gumegume.

**Mwanamume ni Mpenda Starehe**

Suala la mwanamume kusawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda sana starehe, linajitokeza katika kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili. Mwanamume anaonekana kuwa ni kiumbe ambaye anapenda kupata starehe hata ikiwa ni kufa na kupona mpaka astareheke. Jambo ambalo huwa tunajiuliza ni kuwa, hivi mwanamume huwa anafanya starehe yeye peke yake au kwa kushirikiana na wanaumke? Jibu ni kwamba, mwanamume hufanya starehe kwa kushirikiana na mwanamke.

Hata hivyyo, anayeonekana kuwa ni mpenda starehe ni mwanaume na si mwanamke. Hii ni elementi ya mfumo dume wa kiafrika ambapo mwanamke sharti abaki nyumbani na kuwatunza watoto lakini yeye mwanamume huzurura sehemu zote atakazo na kurudi nyumbani wakati wowote anaotaka. Pia, mwanamke hana uhuru wa kujichagulia mwanamume mwingine asiye bwanake alakini yeye mwanamume akienda sehemu fulani kujisherehekea, humpata mwanamke mwingine ambaye siye mkewe na hapo hamna shida kwa sababu mwanamume hawezi kuwa wa mke mmoja (kulingana na imani ya Kiafrika). Katika riwaya ya Msururu wa Usaliti tunaona mwanamume akisawiriwa kama kiumbe mpenda starehe au raha kama ifuatavyo:

Kutokana na mafanikio yake kazini, aliuza garinlake alilokuwa nalo mwanzoni akanunua gari mpya chapa ya Trooper. Pia alibadilisha samani katika nyumba ya kupanga alimoishi, akanunua ma,kochi, kitanda, meza, viti, Runinga na mazulia yaliyoendana na mtu wa cheo chake. Lakini pamoja na maendeleo yote haya Agutu alihisi kwamba pesa hazitoshi akahitaji nguo mpya za bei kubwa kila uchao. Alitaka kwenda kutengeneza nywere za weledi waliolipisha pesa nyingi sana kwa huduma zao. Gri lake kubwa lilikuwa bahari isiyoshiba maji hata baada ya mito kadha kuimiminia, mafuta yake yalimgharimu pesa nyingi. Pia, alitaka kujiburudisha mara kwa mara na marafiki zake katika vilabu vya watu wa tabaka lake. Kweli bandu bandu humaliza gogo, mambo haya yaliumega mshahara wake mkubwa usibaki chochote………..Badiliko hili lilitokea kufuatia maingiliano yake na baadhi ya wateja wake matajiri.si Dkt Makau ambao akaunti zao zilingia pesa kama matone ya maji………..(Uk 148-149).

Maneno haya ni uthibitisho tosha kuwa wote mwanaume na mwanawake wanashiriki katika starehe. Dondoo halionyeshi kwamba ni mwanamume pekee ndiye ambaye anashiriki katika starehe. Tena, dondoo linaonyesha kuwa mwanaume ndiye ambaye ametoa fedha kwa ajili ya kugharamia starehe baina yake na wateja (Wanaume) maana ndio waliokuwa wakinunua mwanamke(Uthibitiisho Uk 148 mshr 24) mwandishi anaposema "…. maingiliano yake nabaadhi ya wateja wakematajiri…." Hapa inathibitisha kwamba wanaume ndio Katika uhalisia, daima mwanamume ndiye ambaye hutajwa kuwa ni mpenda starehe na ndiye hushawishi mwanamke washiriki katika starehe. Huu ni mfano mzuri wa namna mfumo dume unavyofanya kazi katika jamii hususani katika kumkandamiza mwanamke kwani yeye haruhusiwi kujistarehekea mwenyewe endapo bila mwanamume.

Alianza na Owawa. Huyu alikuwa mkurungenzi wa kampuni ya ujenzi wa barabara ambayo mara nyingi alipewa kandarasi na serikali kujenga barabara kote

**ISSN: 1813-4270**
**Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44**

nchini.Owawa alikuwa tajiri mkubwa, ndiye aliyemfunza agutu utamu wa ziara za kitalii nje ya nchi.Walizuru Ushelisheli,Moris, Afrika kusini……Aidha walikuwa wakichukuwa livu kazini na kwenda kustarehe kwenye hoteli za fukweni kwa siku kadha.(Uk 150)

Dondoo hili linaonyesha kuwa Owawa ambaye ni mwanamume mtajiri anapenda mambo ya starehe, anazurura huku na kule pamoja na Agutu kwa kumfadhili na kumlipia gharama, Owawa alikuwa ni mtu wa starehe na alipenda ziara za utalii. Hata hivyo, tunaona kwamba, mwanamume ndiye anayemshawishi mwanamke nah ii ina maana kwamba mwanamke ni chombo cha starehe kwa mwanamume, bila yeye starehe haiwezi kukamilika.

Katika jamii ya kiafrika kuna ile dhana kuwa mwanamke ni kiumbe wa kununuliwa katika shughuli zote za kijamii kama vile kulipwa kwa mahali kwa wazazi wake, hushawishika na pesa kwa ajili ya ngono nakadhalika. Ile dhana ya kwamba ni lazima amtegemee hata katika baa akisubiri apate mwanamume wa kumnunulia pombe inadhalilisha ujidunishaji umeotawala fikra za jamii. Hii inawabomolea wanawake heshima na kudhaurauliwa kwa kejeli na kashifa kuwa wao ni wapenda starehe.

**Mwanamume ni Kahaba**

Dhana ya kwamba mwanamume ni kiumbe Kahaba si ngeni katika ulimwengu wa fasihi na hata katika masikio ya watu katika jamii (Ramadhan, 2013). Kahaba ni mwanamume ambaye anakuwa na mahusiano na wanawake nje ya ndoa kwa malengo mbalimbali ikiwemo kupata fedha na kuridhisha nafsi. Wapo wanaume ambao wameoa kwa kufuata taratibu zote za kijamii, kidini na kisheria lakini hutoka nje ya ndoa zao na kuwa na mahusiano na wanawake wengine. Pia, wapo wanaume ambao hawajaoa bado na hivyo huamua kufanya biashara ya ngono kwa kununua wanawake ili waweze kustarehesha na kuridhisha miili yao. Maelezo haya yanabainisha Ukahaba unaofanywa na mwanamume si wanawake peke yake kama inavyojulikana katika jamii bali wapo wanaume ndani yake. Mwanawake hawezi kuwa Kahaba bila mwanaume anayehitaji

**METROPOLITAN JOURNAL OF SOCIAL AND EDUCATIONAL RESEARCH**
**ISSN: 1813-4270**
**Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44**

ngono. Hii ni sahihi kusema kwamba, wote mwanamume na mwanaume ni Kahaba (Sengo, 2009). Mwandishi ameisawiri hali hii na hapa anasema:

Lakini Mbogo alikiuka mipaka ilipoyaleta nymbani.Alimbaka mhudumu wake wa nyumbani.Msichana aliyefanyiwa haya alikimbilia kwa wazazi wake. Makena alipouliza, Mbogo alimjibu kwamba hakufahamu kwa nini mhudumubaliondoka ghafla.Makena alituhumu kwamba lazima kulikuwa na jambo. Alimfuata msichana kwa wazazi wake na kumdadisi. Alimfichulia yote. Huu ulikuwa mshale wa Usaliti ambao ulishinda mwingine wowote kuwahi kurushwa na mumewe. Ulimtia wazimu, akarudi nyumbani na kuzusha zogo kubwa.(Uk 207)

Dondoo hili linadhalilisha ukahaba wa Mbogo kwa kumrazimisha katika mapenzi mhudumu wake wa nyumbani. Kitendo hiki kilisababisha kashifa katika ndoa ya Mbogo na Makena karibu ndoa yao iharibike. Katika jamii, jambo hili halichukuliwa kama kitendo kiovu sana mwanamume kufanya mapenzi na mwanamke ambaye si mke wake bali jambo linalochukuliwa kama kitendo kiovu ni mwenendo wa mke wa mtu akishikwa ana kwa ana akifanya ukahaba. Aidha kuna imani kwamba mwanamume anatarajiwa kuoa wanawake zaidi ya moja ikiwa ana uwezo wa kifedha wa kuwahudumia.

Hapo basi tunapata mantiki ya kuendeleza mfumo dume unaomkandamiza mwanamke kwasababu huenda naye huwa na hisia za kupata wanaume zaidi ya mmoja ambaye ni mumewe rasmi. Katika dondoo lifuatalo tunavumbua kwamba katika Riwaya hii ya Msururu wa Usaliti, mwanamume amesawiriwa kama kahaba.

Aidha walikuwa wakichukuwa livu kazini na kwenda kustarehe kwenye hoteli za fukweni kwa siku kadha. Tatizo la Owawa lilikuwa mkewe ambaye alikuwa pilipili. Kwa hali hii, ilibidi ajifiche sana wakati akivunja sheria ya ndoa. Hata kwenda ziara za nje ya nchi ilikuwa njia mojawapo ya kujificha. Lakini maficho ya nje yalihitaji mipango mikubwa ambayo haikuwezekana kwa wingi kukidhi utashi wao wa kukutana. Kwa sababu hii, ilibidi maficho ya ya Agutu na Owawa yawe jijini. (Uk 150).

Maneno ya dondoo hili yanathibitisha kuwa Owawa ambaye ni mume wa mtu alikuwa ni mwanamume mwenye uhusiano wa kimapenzi na Agutu ambaye ni kiguna njia. Hii ni ishara kuwa bwana huyu alikuwa Kahaba Kwa hiyo ni sawa na kusema kwamba Bwana Owawa licha ya kuoa na kuwa na watoto naye alikuwa ni Kahaba aliyekuwa na uhusino na wanawake wengine tofauti na mke wake. Katika uhalisia hivi ndivyo mambo yanavyofanyika ambapo wapo wanaume wanaotoka nje ya ndoa zao na kuwa na wanawake wengine wanaojulikana kwa jina maarufu la nyumba ndogo. Hupeleka mahitaji yote muhimu katika nyumba ndogo hiyo na wakati mwingine mke wa ndoa hukosa mahitaji muhimu kwa sababu ya mke mdogo Malaya huwa na mahitaji makubwa zaidi. Huu bila shaka ni Ukahaba wa hali ya juu unaofanywa na wanaume lakini daima mwanamke ndiye ambaye analaumiwa (Lyatuu, 2011). Lazima ifike mahali jamii itambuwe kwamba suala la Ukahaba katika jamii si la mwanamke peke peke yake bali ni la watu wote wakiwemo wanaume na wanawake.

Hii itasaidia hata katika harakati za kukomesha Ukahaba katika jamii. Leo hii tunaona namna serikali inavyojitahidi kupambana na wanawake Kahaba wanaojiuza katika miji mikubwa kama Mbale, Jinja, Kmpala, Mbarara, Masaka, na kwingineko kwa madereva ili kupunguza maambukizi ya virusi vya Corona lakini hawafanikiwi kwa sababu inamuona mwanamke kuwa ndiye Kahaba na kusahau hata wanaume ndio Asilia kuu ya uendelezaji wa taasisi ya Ukahaba.

Ilifaa jitihada hizo ziende mbali zaidi na kumhusisha mwanaume ambaye ndiye mdau mkuu katika masuala ya Ukahaba. Jitihada zifanywe kwa kuwalenga wanaume na wanawake na si jinsia moja tu ya uke kama vilivyo katika jamii.

**Mwanamume ni Kiumbe Mwovu**

METROPOLITAN JOURNAL OF SOCIAL AND EDUCATIONAL RESEARCH
ISSN: 1813-4270
Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44

Katika riwaya ya Msururu wa Usaliti, Mwanamume anasawiriwa kuwa ni mwovu wa aina tofautitofauti ikiwemo kuwatoa watu maishi juu ya tamaa ya utajiri, usaliti wa ndoa kwa ajili ya kupata starehe, mlevi, mbakaji,na mwizi wa mali ya wenzake. Katika jamii inajulikana kuwa ni kutokana na uovu huu wa mwanamume ndio maana leo hii kuna matatizo mengi kama maradhi, njaa, ujinga, chuki, uchoyo, fitina na kadhalika.

Hii ndiyo inayowafanya wanajamii kuwa na imani kwamba mwanamume ni baba wa maovu katika jamii. Mwandishi anaonekana kuungana mkono na mtazamo wa wanajamii ambapo naye amemsawiri mwanamume kama kiumbe ambaye ni muovu na anaweza kuleta maafa katika jamii. Katika dondoo lifuatalo anasema:

… Uchungu wote wa dhiki za maisha yake ukamrudia. Ukamgeuza kuwa samba mla watu. Usiku wa manane, samba huyu akanyata mpaka kwenye kibanda cha Igweta. Akasukuma mlango. Mlango ukafunguka. Mzee alikuwa amelala.Simba akamshika shingoni kwa mikono ya chuma na kuifinya kama mtu afinyavyo chawa katikakati ya vidole.Shingo dhaifu ya Igweta haikuhitaji kufinywa sana. Muda si muda mwili wake ulilegea, akakata roho.Baada ya kumaliza, samba alifuta alama zote za uwindaji wake. Keshoye alikwenda kwa chifu kurepoti kwamba Igweta amekufa.Wote wawili wakakubaliana kwamba bila shaka alikufa kwa kutokana na uzee.Chifu aliyekuwa pia mkewe Mbogo, hakuhutumu uhalifu wowote (Uk 65).

Dondoo hili ni mfano mzuri wa namna mwanamume alivyokuwa kiumbe mwovu ambapo tunaona Mbogo akimtoa maisha Mzee Igwete jilani yake ili apate kuipa ardhi yake bila kizuizi.

Anamwendea usiku wa manane katika kibanda chake alimokuwa akilala peke yake na kumtoa maisha taratibu na hamu ya Mbogo ilipanda kiasi kwa lengo la kupanua shamba lake kwa kuongezea lile la Igweta. Chifu ambaye ni mwanamume anafitafita

METROPOLITAN JOURNAL OF SOCIAL AND EDUCATIONAL RESEARCH
ISSN: 1813-4270
Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44

mambo kuhusu ukweli wa kifo cha Mzee Igweta . Hii ni dhalili kwamba mwandishi Mwenda Mbatiah amemsawiri mwanamume kama miumbe mwovu asiyejali binadamu hata kamwe bali amejaa matunda ya ubinafsi wa hali ya juu.

Katika jamii ya leo wapo wanaume watajiri ambao wana sifa kama hii ya kuwatoa maisha maskini kutokana na wivu au wakati mwingine tama ya utajili inayowapanda. Hii ni tabia mbaya na haifai kuvumiliwa hata mara moja katika jamii. Pia, Mbogona na Makanika wanapanga kifo cha Makena katika dondoo lifuatalo:

"Aliyeajiriwa kutekeleza mauaji alikuwa Mdudu-Makanika wa zamani jeshini, aliyepigwa kalamu kwa kuiba vipuri. Sasa alikuwa amejificha katika biashara ya kuuza vipuri lakini ukweli ni kwamba alikuwa mwizi wa magari.Genge lake liliiba magari, kuyavunjavunja na kuuza sehemu yake kama vipuri. Lori lake aina ya Mercedez Benz alilonunua jeshini, na alilolibatiza jina la kifaru, ndilo alilotumia katika mradi wa kumwangamiza Makena. Alimwelezea mwajiri wake hiv,Toyota Corolla ya Makena itakuwa inatelemka kwenye barabara hii ikiwa nyuma ya kifaru. Katikati ya mteremko kigari hiki kitakuwa kinabingirika kama jiwe kutoka mlimani. Kumbuka nitakuwa nimeharibu breki zake kwa sili. Ghafla nitafunga breki katikati ya barabara. …………………..dereva wa kigari hiki akipona, njoo uchukue pesa zako.Polisi nitazungumza nao….(Uk211)

Dondoo hili linahakikisha kwamba Katika jamii ya leo wapo wanawake wenye tabia ovu kama hii ambapo hukusanya huwafanyia njama wake zao na kuwatoa maisha ili wapate kutekeleza kazi zao za majendo pia chafu. Hii ni kwa sababu wake zao huzipinga kazi zilizochafu hasa zile za kuwanyanganya mali zao watu wengine ili kutajirika na kuuona kama mwenendo mbaya unaoweza kusababisha laana kwa uzazi wa familia hiyo. kwa kuwa na msimamo huo huo, baadhi ya wanaume huanza kuwatambua wake zao kama vipingamizi vya maendeleo na kwa hiyo huamua kuwatoa maisha.

**Mwanamume Kama Mchapakazi**

Mwandishi Mwendah Mbatiah amemsawiri Mwanamume kama mtu ambaye mchapa kazi nyingi za ujasirimali tangu karne na karne pia hunufaiki na ujasiriamali huo. Ujasiriamali ni msamiati uliopata matumzi hapa Uganda hasa mji wa Mbale katika miaka ya hivi punde 2010 na kuendelea lakini shughuli za ujasiriamali zimekuwepo kwa karne nyingi. Wanaume ndio wafanyakazi wakubwa wa kutumainiwa katika shughuli za kuzalisha mali na maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla, ufugaji, ujenzi, Ubawabu, Ulinzi, biashara kubwa nakadhalika na kipato kinachopatikana hufanya kazi mbalimbali za maendeleo kama kuwalipia ada wato,nguo, kununua ardhi na matibabu wakishikwa na ugonjwa.

Katika riwaya ya Msururu wa Usaliti tunaona mfano mzuri wa namna mwanamume alivyomchapa kazi wa kutumainiwa na familia yake. Mwandishi anasema:

…Baadaye Mbogo alijenga nyumba ya Mbao akahamia humo. Alijiuzulu ile kazi ya bwana Mark akawa Mkulima wa kahawa Mbogo aliendeshwa na mambo mawili kama vile mafuta yaendeshavyo gari: Kushinda Adui Umaskini-ndilo lililokuwa la kwanza. La pili lilikuwa kufuta  doa la kudharauliwa kijijini.Alijiambia kwamba kwa kuchapa kazi , angelilazimisha kijiji kumtambua.

Alilima kama mtu aliyekuwa akipigana vita na ardhi. Mibuni kwenye shamba alilonunua ilikuwa dhaifu kwa kusakamwa na magugu. Aliyashambulia kwa ghadhabu. Ilikuwa kazi ya kila siku; mchana kutwa, kwa miezi mitatu. Baada ya kuufyeka msitu wa magugu, kazi nyingine zilizobaki zilikuwa rahisi kwake. Alipiga matuta makubwa kama vilima. Kisha akanunua samadi nyingi kutoka kwa wafungaji….(Uk 58).

Katika dondoo hili kunaelezwa kuwa Mbogo alikuwa ni mwanamume mchapakazi aliyefanya kazi mashambani ili apate kuepukana mambo wakuu waili yaani adui ambaye ni Umaskini na ndoa ya kudharauliwa kijijini.

. Huu ni mfano mzuri unaonyesha kuwa wanaume si watu wa kukaa nyumbani kusubiri mambo kujitenda bali wanajitahidi wafanye kazi na kuleta chakula nyumbani huku

mke akiwa amejibweteka. Kitendo cha mwanamume huyu kufanya kazi ya Ulimi ni kwamba mwanamume si kiumbe tegemezi kama vile mwanamke, kwani anaweza kufanya kazi na kujipatia mapato ya kukidhi mahitaji yake ya maisha na familia yake kwa jumla.

..Hivyo basi baada ya kuitupilia mbali kazi ya askari wa jela kama vile mtu anavyotupilia nguo nzee iliyoraruka anaponunua mpya. Biashara ya Kipanga ilivyoleta pesa kwa wingi kama mchanga wa bahari, miaka miwili ilimtosha kuzaliwa upya, kutoka askari wa jela aliyekuwa analipwa shilingi elfu tano kwa mwezi. Sasa alikuwa milionea aliyeweza kuwaajiri maaskari elfu moja. Hivi ndivyo mamelionea wa kiafrika walivyozaliwa..

Dondoo hili linaonyesha kwamba Kipanga ni mwanaume mfanya kazi na bidi kwani anafanyajuu chini kuepukana hadhi ya umaskini kwa kufanya biashara ili kuzidisha uzalishaji wa mali. Mwanamume wa leo anatakiwa kupatiwa mtaji wa kutosha ili aweze kuendesha shughuli zake vizuri na zikuwe zaidi. Hivi leo, wanaume ndio wanaolipa ada za watoto wao shuleni na kuwapatia mahitaji yao yote ya msingi.

**Mwanamume kama mwizi**

Mwandishi wa riwaya ya Msururu wa Usaliti amechora jinsia ya kiume kama inavyoshirikiana na vitendo vya wizi. Hapa ni kutunia njia yoyote na kunyakuwa mali ya mtu au watu bila ruhusa ya mwenyewe. Katika riwaya hii kuna wanaume mbali mbali wanaohusika na vitendo vya wizi wa vitu vya wenzao, na halikadhalika hupata athara kutokana na vitendo hivyo. Mwenendo wa wizi husababishwa na tamaa ya kutaka utajiri wa haraka haraka, hapo basi humalizia wamejitumbukiza katika jangwa la ouvu ili kutimiza tamaa ile ile.

Aliitisha mkutano wa wanachama wote akatoa wazo ambalo alikuwa nalo siku nyingi, Wazo la kuanzisha duka la mikopo la wakulima. Duka ambalo lingekopesha wakulima vitu walivyohitaji kama vile mbolea, majembe na dawa za mimea yao. Wangelipa pole

ISSN: 1813-4270
Vol. 2 Issue 4, July - 2023, Pages: 11-44

pole kwa kukatwa pesa walizolipwa kwa kahawa zao. Aliwaelezea kwamba wazo hili lilifanya kazi vizuri sana katika vyama vingi vya ushirika alivyowahi kutembelea wakulima walifurahishwa na wazo hilo. Akaidhinishwa kutoa shilingi milioni tano kutoka kwenye akaunti ya chama ili kujenga duka na kulijaza bidhaa. Mbogo alifyatuka kama mshale uliorushwa na mwindaji hodari, alilitengeneza gari lake, aina ya Land Rover. Lilitiwa vipuli, likapigwa rangi , likawa jipya. Halafu akatoa zile pesa kutoka akaunti ya wakulima. Halafu akasafiri kwenda mji mkuu ambako alikaa kwa juma zima. Alinunua kiwanja kikubwa na kuanza mradi wa kujenga nyumba ishirini za kukodisha………..wachungiuzi walifichuwa kwama mbog aliwapuuza wanakamati na kufanya mambo peke yake. Pili alishatoa pesa zote za mradi na kuzitumia kufanya mambo yake ya kibinafsi…….(Uk 68-69).

Kulingana na dondoo hili, inathibitishwa kwamba Mbogo aliwapuuza wanakamati na kuiba peza za wakulima. Pesa hizi baada ya kuzipata alizitumia kufanya mambo yake binafsi kama vile kulitengeneza gari lake na kujenga nyumba za kukodisha mjini. Pia kuna mwanamume mwingine ambaye amesawiriwa na kama mwizi katika dondoo hapo chini;

kipanga alinyamaza akadodoa macho kama mtu aliyekutana ana kwa ana na samba. Sasa alitambua kwamba alielekea kuzitambua sili zake. Aliingiwa na hofu. Hakujua aendelee vipi

“Labda …….tuaache haya maneno ya wanasiasa,” alijaribu kubadilisha mbinu. “Ile sehemu unayopanda miche…. nataka aa…unirudishie. Yaani uondoke pale kwa sababu nataka kujenga.”

“Sikiliza kipanga”, Kage alisema kwa sauti thabiti  “Hakuna haja ya kutafuna maneno.ile si ardhi yako kwa hiyo huwezi kuniagiza kuondoka pale. Ni ardhi ya Umma uliyosaidiwa na

Waziri wa kawi kuinyakua.”……

Dondoo hili ladhihirisha wizi wa ardhi ya Umma na viongozi hasa wale wa chama tawala wanaojulikana ncnhini kote. Baada ya waziri aliyemsaidia Kipanga kunyakua ardhi hiyo kutambua kuwa ameiazima Kage ambaye ni mpinzani wa mwenendo huo, alimwaagiza amfukuze. Lakini Kipanga mambo yakamgeukia pili pili alipomtaka kutimiza sharti la Waziri akamkuta Kage ameshapata fununu ya kili sili juu ya umiliki wa ardhi hiyo.

Katika jamii ya leo, kuna viongozi ambao wanalaumiwa kwa unyakuzi wa ardhi ya Umma na za watu binafsi. Jambo hili limeegemea sana mkondo wa siasa ambapo wale viongozi waliomo katika Chama tawala huchukua nafasi na vyeo wanavyo kunyakua ardhi ya umma na mali ya watu wa tabaka la chini.

Lakina kwa kuwa hakuna sili ya wawili, wanasiasa kutoka cha wamefanya hatua taratibu za kuchunguza wizi wa aina hii na kuupiga vita mno iwezekanavyo ili kitendo kama hiki kipate kutoweka kifutwe kwenye jamii.

**Mwanamume kama mwenye mamlaka**

Katika kazi nyingi za kifasihi mwanamume hupewa nafasi ya kwanza kwa kumsawiri kama mwenye utawala wa kila kitu katika jamii hata maamuzi ya nyumbani. Katika riwaya ya Msururu wa Usaliti mwandishi amemchora mwanamume kama mwenye mamlaka zaidi ya mwanamke pale ambapo hata mali nyumbani huwa chini yake maana mwanamke hamiliki chochote kuhusu mali. Angalia dondoo lifuatalo.

Hatimaye Naito alipata fursa ya kuzungumza baada ya wanawake wengine kadha kufanya hivyo. Alimweleza Kage kuwa kiini cha matatizo ya wanawake wa vijijini ni umaskini. Kwa kiasi kikubwa, hali hii ilisababishwa na na Mila na desturi zilizohusiana na Umilikaji.Rasilimali kuu ilikuwa ardhi.Nayo ilikmilikiwa na wanaume. Mwanamume akiwa mwenye shamba anaishiwa kuwa mwenye chochote kitokacho shambani. Mke na watoto walikuwa kama wafanyikazi wake.Alichofanyia mapato yaliyotokana na mazao ya shambani kiwe kizuri au kibaya ilikuwa ni chini yake.(Uk 202)

Dondoo hili linadhihilisha kuwa mwanamume ndiye peke yake aliye na dira ya nyumbani na mali yote nyumbani. Maana mwanamke na watoto ni kama wafanyi kazi, thamani yao ni duni kiasi kwamba haitambuliki. Pia katika dondo lifuatalo tunaona kuwa mwanamke amesawiriwa kama mkwasi zaidi ya mwanamke.

“Mbogo na Makena walipooana, ndoa yao ilisimama juu ya mhimili imaraya mapenzi. Kage alipozaliwa, mhimili mwingine ukaongezewa. Walipenda binti yao, wakashirikiana kumpa malezi bora kadri ya uwezo wao. Mara, wimbi kubwa la mabadiliko likawakokota hadi mji mkuu. Mbogo alizidi kutajirika, halafu akaingia katika siasa. Pesa na madaraka ya kisiasa yakazua ulevi mkubwa wa wanawake. Badiliko hili lilimshangaza na kumsikitisha Makena.Alimeza machungu mengi, akayaficha maovu ya mumewe ili yasifikiwe na na macho ya walimwengu”(Uk 206).

Dondoo hili latumbulisha mfumo dume. Mwandishi anasema kwamba baada ya kufika mjini akazidi kutajirika, ingawa walikuwa mume na mke, yeye mke hatambuliki katika utajiri bali huzungumzia juu ya mwanamume peke yake. Hii ni ishara kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe duni lakini mwanamume amechorwa kama kiumbe halisi pia cha thamani na kupewa sifa chanya.

Katika jamii ya leo pia, kuna mila na desturi ambazo humpa mwanamume mamlaka zaidi ya mwanamke. Katika baadhi ya familia suala hili limekuwa nguzo ya maendeleo lakini katika familia nyengine limekuwa mwamba wa kukwamisha maendeleo. Hii ni kwa sababu mhimili huu wa humpa mwamamume uhuru wa kutumia mali jinsi atakavyo bila kutegemea au kujali shauri la mwanamke. Ndiyo maana wanaume wengi wameishia katika dimbwi la ulevi, umaskini ukafunika familia, ada ya watoto huwa vita, na chakula huwa kukwepa mti wa miba. Hii ni kwa sababu wanaume huuza baadhi ya rasilimali na kuchukuwa fedha katika Umaya na mabaa na mwanamke hana lolote la kuchangia kwasababu mila na desturi humrazimisha kutosema lolote.

**Mwanamume ni kiumbe Mwenye huruma.**

Mwanamume ni kiumbe ambaye anatazamiwa kuwa na huruma ya hali ya juu hasa kwa mtotowe. Mtazamo huu unatokana na maumbile ya mwanamume kuwa ni kiumbe mtulivu mwenye huruma na asiyekuwa na makuu. Pia, mfumo dume katika jamii umemfanya mwanamume kuwa ni mtu wa daraja la kwanza ikilinganishwa na mwanamke ambaye ni daraja la pili. Hali hii imemfanya mwanamume kuwa ni mtu wa huruma. Hata hivyo, si wanaume wote ambao wamekuwa na sifa hii ya huruma katika kila kitu lakini bado wanaume wengi ni wenye huruma. Mfano mzuri wa mwanamume mwenye huruma ni Mbogo ambaye alikuwa ni Mumewe Makena na babake Kage. Mwandishi anasema:

“Baada ya kufikilia kwa muda, Mbogo alitoa pendekezo jingine. Alitaka kumfungulia Kage akaunti na kutia humo shilingi milioni mbili kwa matumizi yake wakati akitafuta kazi. Kage aliona hii kama kamba ya kumfunga kwa babake. Alivyouthamini uhuru wake, ailibidi aulinde kwa kukataa kufungwa kamba hii…… “Unasemaje Kage?”Mbogo alimaka. “Huhitaji pesa?sikuelewi. Sikuelewi hata kidogo. Nilifikiria kwamba ukimaliza masomo utakomaa kimawazo kwa maranyingine umeyavunja matarajio yangu.” “Samahani kama ndivyo unavyoona baba……

Dondoo hili linazungumzia namna Mbogo anavyomhurumia Bintiye Kage na kutaka kumpa pesa kama mwananwe ule wakati kabla ya kuajiriwa popote ili kuwa na uwezo wa kujitegemea. Ingawa Kage ana msimamo thabiti wa kutomtegemea babake, Mbogo anamhurumia mwanawe maana hataki ateseke kama yatima babake akiwa bado uhai. Kwa hiyo inathibitisha kwamba mwandishi Mwenda Mbatiah amemsawiri mwanamume kama kiumbe mwenye huruma.

Katika ulimwengu wa leo wapo baadhi ya wanaume wenye huruma kama Mbogo lakini asilimia kubwa ya wanaume hawana huruma kama huyu. Hii ni kwa sababu katika maisha ya siku hizi kumekuwepo na kampeni nyingi za kuwahamasisha wanaume kutia

maanani utamaduni wa kiafrika kwa kusimama katika nafasi zao za udume katika jami wasije wakadharauliwa na jinsia ya kike. Suala la mwanamume kujipaza kimamlaka ni haki yake ya msingi na haitakiwi kusubiri mpaka mtu fulani atoe ruhusa. Hivyo, kisa hiki cha Mbogo ni funzo kwa wanaume wote kuchukuwa uwajibu wao kama baba, ubaba haudaiwi bali hubebwa na kutekelezwa kwa kuajibika.

**Usawiri wa Mwanamume katika Msururu wa Usaliti na Uhalisia Wake kwa Jamii**

Mwanamume amesawiriwa katika nafasi mbalimbali ndani ya riwaya ya Msururu wa Usaliti ambapo kwa kiasi kikubwa imeonekana kuwa mwanamume ni kiumbe ambaye anafanya jitihada kuhifadhi nafasi yake katika jamii ya Kiafrika inayompa mamlaka na ufuhali zaidi ya mwanamke. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa mwanamke ni kiumbe tegemezi kwa mwanaume, mwanaume ni kiumbe mpenda starehe, mwanamume ni Kahaba, mwanamume ni kiumbe mwovu, mwanamume ni kiumbe mwenye huruma na mwanamume ni kiumbe mchapakazi. Kwa hakika, riwaya ya Msururu wa Usaliti imemsawiri mwanamume katika hali ambazo tunaziona zikitokea hata katika maisha halisia ya jamii ya kiafrika. Zipo baadhi ya jamii ambazo zinamtazama mwanamume kama kumbe jasiri, ilhali mwanamke katazamwa kama kiumbe asiyeweza kufanya kazi na kujitegemea.

Hawa ni baadhi ya watu ambao huwafanya wake zao kuwa ni watu wa ndani wasioruhusiwa kutoka nje kwenda kufanya kazi. Sababu kubwa ya kufanya haya ni wivu tu ambao huwakumba baadhi ya wanaume wakidhani kuwa kuwaruhusu wake zao kwenda kufanya kazi kutasababisha wapate wanaume wengine. Kiuhalisia tumeona kuwa jambo hili kwa sasa limepungua mno na hata kama wapo ni wanaume wachache wenye mtazamo kama huo. Wanaume wengi wanawaruhusu wake zao kufanya kazi ili kupata kipato kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya familia.

Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa mwanamume anasawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda sana starehe. Mwanamume anasawiriwa kuwa ni mtu ambaye anapenda starehe za kunywa pombe na kushiriki ngono na wanwake na kwamba analaumiwa kwa hilo.

Katika utafiti huu imebainika kuwa mwanamume huwa hawafanyi starehe wenyewe bila ya wanawake kwa hiyo wanaume huwa ndio huwa wanawataka wanawake kufanya nao starehe. Pamoja na ukweli huu ni mwanamume peke yake ndiye ambaye anaonekana kama kisababisho cha starehe na hii ni kwa sababu mwanamume ndiye anayefadhili visa vya starehe kwa kulipa chakula na vinywaji huku akimnunulia mwanamke. Mwandishi wa riwaya hii amesimama kwenye msingi wa ubabedume unaopatikana katika jamii kwa kumchora mwanamume kana aliye na Uwezo kamili zaidi ya mwanamke. . Wanaume hutaka kuonekana kuwa wao ni watu safi na wakamilifu na wanawake ndio wakosefu na wenye matata. Hii si sahihi hata kidogo bali katika uhalisia tunatambua kuwa starehe ni kitu ambacho kinapendwa na wanaume na wanawake pia.

Matokeo ya utafiti yanaendelea kubainisha kuwa mwanamume anasawiriwa kama kiumbe ambaye ni mwovu. Hii inajitokeza pale ambapo mhusika anayejulikana kwa jina la Mbogo anavyopanga njama na kumtoa uhai mkewe Makena. Kitendo hiki kinatokea pale ambapo Mbogo anapenda kufanya shughuli za majendo zimezojaa maovu na Makena kama mkewe akajaribu kuingilia kwa kuchangia ushauri wa kumkosoa ili mumewe mpendwa aepukane na hali hii, lakini yeye Mbogo akamwona kama kipingamizi cha maendeleo na ikambidi amtoe maisha ili apate kuendelea na bila kizuizi. Pia twamwona Mbogo akimtoa maisha Mzee Igwete kwa kuvamia na kumkunja shinko usiku wa manane, anamuua na kuchukuwa shamba lake na baadaye akatajirika.

Vitendo hivi havikuwa vizuri hata kidogo na hakipaswi kufanywa na mtu yeyote yule awaye katika jamii. Katika jamii ya Kiafrika pia wapo baadhi ya wanaume ambao kwa

makusudi hutumia njia za hila kuwapotosha wake kwa kuwatoa maisha ili wapate kujinyakulia uhuru wa kuendeleza shughuli zake za starehe. Pia katika jamii, kuna wakwasi wanaowatoa maisha maskini ili kunyanganya mali yao bila shaka.

Aidha, mwanamume amesawiriwa kama kiumbe msaidizi mwenye nguvu kwa hiyo hutia jidihada tele katika ufanikaji wa familia yake yaani mkewe, watoto na kila anayeishi katika familia hiyo. Mwansishi amemsawiri Mbogo kwa kumpesa akanunua gali la kumsaidia katika shughuli zake. Hata katika jamii ya leo, kuna watajili wanaume ambao huwanunulia magari watoto wao hata baada ya kuhitimu na kumaliza misomo yao.

Pia, Mwandishi Mwendah amemsawiri Mwanamume kama mtu ambaye ni mchapa kazi halisi na kutajirika. Katika riwaya hii Mbogo ambaye alikuwa maskini hapo mwanzoni, lakini alipoamua kujitahidi, jitihada zake zikamfulia dafu na kutajirika.

Zaidi ya hayo, mwanamume amechorwa kama kiumbe Kahaba . Kahaba ni mwanamume ambaye huwa na uhusiano na wanawake zaidi ya mmoja au nje ya ndoa kwa malengo mbalimbali ikiwemo kupata fedha na kuridhisha nafsi. Tunamwona Mbogo anavyofanya ukahaba na Agutu, Dkt Makau pia na Agutu, na mtajiri Owawa naye anafanya ukahaba na Agutu. Katika jamii ya leo, pia kuna wanaume wasiothamini miili yao au ndoa zao kwa kujihusisha na wanawake tofoutitofouti. Lakini ukweli ni kwamba matokeo ya vitendo vya ukahaba huwa ni hasi kwa wahusika wenyewe, familia zao na jamii kwa jumla.

## Hitimisho

Kwa jumla, riwaya ya Msururu wa Usaliti ni riwaya ambayo bado inaeleza mambo yenye uhalisia katika jamii ya leo na ni vema ikaendelea kusomwa katika ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini. Riwaya hii imeandikwa na Mwenda Mbatiah mwaka

2011 ambapo mpaka sasa ni miaka 9 (tisa) lakini mambo inayoeleza kumhusu mwanamume yana uhalisia katika jamii ya kiafrika. Kulingana na msimamo wake katika utafiti huu, mwanamke sharti atamue kwamba mwanamume ndiye mungu wake wa pili hapa duniani, asipokuwepo maisha yake huwa maangamizini kwani hawezi kujitegemea yeye mwenyewe bila msada wa mwanamume.

Aidha, kwa upande mwingine, tukiangalia riwaya nzima, tunapata kwamba kweli kabisa mume na mke ni viumbe vinavyotegemeana. kwa mfano wakati Mbogo alipokuwa akigombania kiti cha ubunge, Makena mkewe ndiye aliyekuwa akimsaidia katika mikakati ya kutafuta kula ili mbogo apate kufaulu bila bugudha. Kwa hiyo hapa tunahakikisha kwamba mke na mume ni viumbe viwili vinavyotegemeana. Usasa umebadilisha mkondo wa kijadi unaomfungia mwanamke katika debe la ujinga na hadhi duni kwa kukandamiza haki zake.

Ni vema wanajamii wakaelewa umuhimu wa kila mwanajamii kusikilizwa kabla ya kuchukua uamuzi wa kufanya jambo fulani. Mtenda mabaya alaumiwe kwa matendo yake lakini sio kulaumu jinsia fulani kwa jumla. Hii inatufanya tuhitimishe kuwa elimu kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia ni kitu muhimu ambacho kinatakiwa kuwa endelevu na kisipuuziwe. Hii itaifanya jamii kuishi kwa amani na usawa na kuepukana mkondo wa kijadi unaodunisha jinsia ya kike. Jamii haiwezi kuwa na maendeleo halisi ikiwa kuna fikra za kuidharau jinsia moja na kuinua nyingine. Ni kweli hata kutokana na maandiko takatifu yaani Biblia na Korani, mungu anamsawiri mwanamume katika nafasi ya kwanza na mwanamke katika nafasi ya pili lakini siyo kama ilivyo katika jamii ya kiafrika imeyopita kiasi kwa kumdharau kwa asilimia 98 mwanamke. asimilia.

## Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa taswira ya mwanamume katika riwaya ya msururu wa usaliti kwa kwa hiyo mtafiti anapendekeza utafiti wa baadaye kuchunguza Usawiri

wa jinsia ya kike kwani riwaya ya Msururu wa Usaliti ina wahusika wanaume wanaochangia pakubwa katika ujenzi wa uti wa mgongo wa riwaya hii.

**MAREJELEO**

Armefred, S. (2004) (Mh) Re-thinking Sexually in Africa. Almgrist and wick sell Tryskers.

Aswani, B, Mayaka, G. na Matinde, R. (    ) Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti. Seringeti Educational Publishers. Mwanza, Tanzania.

Berger, c. and Connel, R. (1995), Masculinities. Berckley University of Califonia Press.

Chacha (2013)" Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Nguzo za mama na Mama Ee".

Dorothy (2007) "A Critical Anaiysisi of Patriarchy and Masculinity in Kezilahbi's Rosa Mistika and Kichwa Maji".

Izugbara, C. (2005), Hypothesis on the Orign of Hegemonic Masculinity in Sexuality in Africa Magazine. Lagos African Religion. Sexuality Resource Centre Publishers.

John, G.(1980), Hegemonic Masculinity. United Kingdom; Bethany House Publishers.

Karinge (2013)"usawiri wa ndoa katika Riwaya ya Unaitwa Nani?

Katola, E(2006),"Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika Riwaya za Kiswahili".

Kimmel, M. (2000), The Gendered Society. New Yolk; Oxford University Press.

Kinyua (2011) katika tasnifu yake ya Riwaya ya Unaitwa nani?

Kipyegon (2013)”Nafisi na utambulisho wa Mwanamke katika tamthilia za Natala na Kifo kisimani.”

Kothari C.R. (2008), Reaserch Methods and Techniques. Rajasthan (India); New Age International limited.

Magoma (1997)” Mwamko wa mwanamke katika tamthilia nne za Penninah Muhando”.

Maina (2005) “Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi mbili za Shaaban Robert; "Utenzi wa Haki naUtenzi wa Adili

Maingi (2011), amefanya utafiti wenye mada”Upembezwaji waa

Maobe (2011), katika tasnifu yake ya “Ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe” .

Millet, k (1970) Sexual Policies,Virago press,London.

Mirikau (2011)” Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila K.W; Seserumbe, Pango na Wingu ia kupita”.

Muhanda(2011),”Nafasi ya dini katika ndoa:tathmini ya Utengano na Paradiso.

Mwendah M. (1998), Msururu wa Usaliti. East Africa Education Publishers. Nairobi.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999), Ufundishsaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.Jomo Kenyatta Foundation Publishers. Nairobi.

TUKI. (2004), Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Oxford University Press.Daresalaam,

Tuki (2004) Kamusi ya Kiswahili sanifu.Da-esalam university Press Dar essalam.

Mwenda Mbatiah (1998). Msururu wa usaliti, East Africa Education Publishers Nairobi.

Onyoni(2013)”Usawiri wawahusika wa kike na kiume katika tamthilia za Natala na Mama Ee”.

Pilcher, J. na Imelda, W (2004), 50 Key Concepts in Gender Studies. Sage Publisers. Los Angeies,

Wafula, R. na Kimani N. (2007), Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.Sai Industries Limitted. Nairobi.

Yego (2013), katika utafiti wake “Nafasi ya Mwanamke katika Nyimmbo za Taarab.